UCHAGUZI

Jarida la Tume ya Taifa ya Uchaguzi Toleo Na. 06 Agosti, 2022



MHE. JAJI (R) JACOBS C. M. MWAMBEGELE
MWENYEKITI WA TUME

NEC YAJIZATITI KUWA KINARA KUSIMAMIA CHAGUZI HURU

IFAHAMU TUME

MZUNGUKO WA UCHAGUZI

Mzunguko wa Uchaguzi

Ibara za 42 (2) na 65 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Kifungu cha 12 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 zinaelekeza kuwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ufanyike kila baada ya kipindi cha miaka mitano (5).

Kama ilivyo kwa nchi nyingine duniani, katika kuendesha shughuli za Uchaguzi, Tanzania hutumia utaratibu wa mzunguko wa Uchaguzi ambao umegawanyika katika awamu tatu (3) kama ifuatavyo :-

(i) Kabla ya Uchaguzi;
(ii) Wakati wa Uchaguzi; na
(iii) Baada ya Uchaguzi.

Kabla ya Uchaguzi

Shughuli zinazofanyika kabla ya Uchaguzi ni pamoja na:-

(i) Uandaaji wa bajeti;
(ii) Uandikishaji wa Wapiga Kura;
(iii) Ununuzi wa Vifaa;
(iv) Uandaaji wa Kalenda na Mpango wa Utekelezaji;
(v) Maboresho ya Sheria na Maelekezo ya Watendaji na Wadau wa Uchaguzi;
(vi) Mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi; na
(vii) Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura.

NEC yajizatiti katika Usimamizi wa Chaguzi huru

Na Mwandishi wetu

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Jaji wa Rufaa Mhe. Jacobs Mwambegele amesema Tume yake imejizatiti kuwa kinara wa kuendesha Chaguzi zilizo huru na za haki kwa nchi zinazoendelea na kwingineko duniani.

Jaji Mwambegele ameyasema hayo kupitia maelezo yake yaliyomo kwenye Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Tume hiyo ambao utekelezaji wake ulianza tangu julai mwaka jana ambapo Tume hiyo imejipanga kuwa chombo kinachoaminika katika kusimamia Chaguzi huru na za haki.

Amesema malengo hayo yatatekelezwa kwa kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa mujibu wa sheria kwa manufaa ya Watanzania, vyama vya siasa na Wagombea ili kuhakikisha mchakato wa Uchaguzi unalinda demokrasia nchini.

“Kupitia mikakati mbalimbali tuliyojiwekea Tume yetu imedhamiria kuwa mfano wa kuigwa kwa Tume za Uchaguzi katika nchi zinazoendelea na kwingineko kote duniani katika kusimamia Chaguzi zilizo huru na za haki,” alisisitiza Jaji Mwambegele na kuongeza:

“Tutatekeleza kwa moyo wote maadili yetu ya msingi na kuwajibika kwa chochote tunachofanya, tutadumisha ufanisi siku zote, tutafanya kazi kama timu kwa maneno na vitendo, na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi kadri ya uwezo wetu ili kudumisha uadilifu.”

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Dkt. Wilson Mahera Charles alisema kuwa Tume hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 1993 imeendelea kuwa chombo kinachoaminika katika kusimamia Chaguzi huru na za haki nchini.

Kadhalika, Dkt. Mahera ameongeza kuwa kwa kipindi chote hicho, Tume imefanya maboresho mbalimbali yakiwemo kufanya mapitio ya Sheria, Kanuni na Miongozo iliyowezesha usimamizi wa Uchaguzi ikiwemo Miongozo ya Elimu ya Mpiga Kura.

UCHAGUZI HOUSE

Tume yateua Mbunge Viti Maalum

Na Mwandishi wetu

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika kikao chake kilichofanyika tarehe 9 Julai, 2022 imemteua Bi. Tamima Haji Abass kuwa Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi.

Uteuzi huo umefanyika kwa kuzingatia matakwa ya ibara ya 78(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 86A (6) na (8) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Uteuzi huo umefanyika baada ya Tume kupokea barua yenye Kumb. Na. CEB.137/400/02A/10 ya tarehe 12 Mei, 2022 kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano iliyoandikwa kwa mujibu wa kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kuhusu uwepo wa nafasi wazi ya Mbunge wa Viti Maalum wa Chama cha Mapinduzi kutokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama.

Jina la Bi Tamima limetokana na orodha iliyowasilishwa awali na Chama cha Mapinduzi wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Baada ya uteuzi huo kufanyika, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dkt. Wilson Mahera Charles alitoa taarifa kwa umma juu ya uteuzi huo na kwa mujibu wa taratibu Tume ilitoa taarifa kwa Spika wa Bunge, Katibu wa Chama cha Mapinduzi na uteuzi huo kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.

Tume ya Uchaguzi Sudani Kusini yafanya ziara Tanzania

Na Mwandishi wetu

Maafisa 11 kutoka Tume ya Uchaguzi na Ofisi ya Vyama vya Siasa kutoka Sudani Kusini wamefanya ziara ya kimafunzo katika Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi zilizopo Njedengwa, jijini Dodoma.

Ujumbe huo ambao ulipokewa na Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Nassoro Shemzigwa, uliongozwa na Katibu Mtendaji wa Tume hiyo, Bw. Yohanes Amum Nyiker ambaye aliambatana na Mtendaji Mkuu wa Baraza la Vyama vya Siasa la nchi hiyo Bw. James Akol Zakayo.

Katika ziara hiyo, wageni hao kutoka Sudani Kusini walipata taarifa fupi ya shughuli za Tume na kupata fursa ya kupata uzoefu wa namna Tume inavyotekeleza majukumu yake ya kusimamia

Uchaguzi.

Akizungumza mara baada ya kupokea taarifa na uzoefu wa Tume katika kusimamia Uchaguzi wa Tanzania, Bw. Nyiker aliishukuru Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mapokezi mazuri na uzoefu walioupata na kukiri kuwa hawakukosea kuichagua Tume hiyo kuwa miongoni mwa Taasisi walizopanga kuzitembelea katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Bw. Nyiker alisema ziara yao ya mafunzo pia wameifanya katika nchi za Ghana, Tanzania na Botswana ikiwa ni kutafuta uzoefu na mbinu mbalimbali za kufanya Uchaguzi ulio bora, wa wazi na uliojaa weledi.

“Tumekuja kujifunza kwenu, tupo katika kipindi cha mpito na Tumechagua nchi za Ghana, Tanzania na Botswana kwa kuwa zina vitu vya kujifunza na tumevutiwa na mfumo wenu wa uendeshaji Uchaguzi,” alisema Bw. Nyiker.

Aliongeza kuwa endapo watachukua mfumo wa uendeshaji Uchaguzi wa Tume ya Uchaguzi ya Tanzania basi wana uhakika watakuwa na ufanisi mkubwa katika uendeshaji wa Uchaguzi Sudan Kusini hivyo, wameuomba uongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendelea kuwapa ushirikiano.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi aliwaahidi wageni hao kuwa Tume yake ipo tayari kushirikiana nao ili kuhakikisha kuwa nchi ya Sudani Kusini inakuwa na chombo chenye weledi cha kusimamia Chaguzi huru na za haki katika nchi hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bw. Nassoro Shemzigwa aliyekaa katikati akiwa na Viongozi wa Tume pamoja na wageni kutoka Tume ya Uchaguzi ya Sudani Kusini wakati wa ziara yao katika makao makuu ya Tume jijini Dodoma hivi karibuni

Matukio mbalimbali ya ziara ya Wageni kutoka Tume ya Uchaguzi ya Sudani Kusini walipotembelea Ofisi za Tume, Njedengwa jijini Dodoma.

Ujumbe UN watembelea Ofisi za Tume

Na Mwandishi wetu

Ujumbe kutoka Umoja wa Mataifa (UN) umefanya ziara kwenye ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) jijini Dodoma kwa lengo la kujifunza mambo mbalimbali ya kiutendaji.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dkt. Wilson Mahera Charles aliupokea ujumbe huo, akiwa na Wakuu wa Idara na Vitengo ambapo aliwaeleza wageni hao mambo mbalimbali kuhusu historia na majukumu ya Tume.

Ujumbe huo wa watu sita uliongozwa na Bw. Akinyemi Adegbola ambaye ni Afisa Uchaguzi Mkuu katika Idara ya Siasa na Masuala ya Amani, Ofisi za Umoja wa Mataifa za Umoja wa Afrika (UNOAU).

Bw. Adegbola aliipongeza Tume kwa kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia misingi bora ya uendeshaji wa chaguzi ambapo imekuwa na historia nzuri ya kushirikiana na wadau wake.

Afisa huyo pia aliipongeza Tume kwa kuwa na jengo la kisasa na kuongeza kuwa wao kama wadau wa Uchaguzi wamefurahi kutembelea ofisi hizo kwani zina mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

Mkurugenzi wa Uchaguzi aliwaeleza wageni hao kwamba

Tume
imeundwa chini ya Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa
Tanzania ya mwaka 1977 ambayo pia imeanisha sifa za wajumbe.
Dkt. Mahera aliwaeleza wageni hao kuwa Katiba hiyo pia imetamka
kwamba Tume katika kutekeleza majukumu yake haitalazimika kufuata
amri au maagizo ya mtu yoyote.
Kwa upande wake Mratibu wa Masuala ya Utawala na Amani wa Shirika
la Umoja wa Mataifa la Mipango na Maendeleo (UNDP) Dkt. Roselyn
Akombe alisema amefarijika kutembelea ofisi za Tume na kwamba
amejifunza mengi ikiwa ni pamoja na jinsi Tume inavyozingatia weledi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dkt. Wilson Mahera Charles akizungumza jambo na ujumbe kutoka UN.

SHAIRI

Jihadhari na KORONA

Na Rashidi Hizza

Ujumbe nawatumia, kwenu walengwa ufike,
Korona imeingia, fanyeni tuiepuke,
Taratibu zingatia, madhara yasikufike ,
Jihadhari na korona ,maisha yana thamani.

Maisha yana thamani,epuka misongamano,
Ni ugonjwa si utani,wala hauna agano,
Jueni tuko vitani, tukabili mapambano,
Ili tushinde medani,taratibu tufuate,

Taratibu tufuate, wasemazo viongozi,
Jueni hali ni tete,kujilinda ufumbuzi,
Kauli mbaya tufute ,dalili tuweke wazi,
Sote tuvuke salama , kwa uwezo wa Manani

Wataalamu wa tiba,wale waliobobea ,
wameshatoa ratiba, mitandao tembelea,
usikukute msiba, ushindwe kuendelea,
zingatia taaluma, uzembe achana nao.

Kwa mapenzi ya mwenyezi , tutaishinda korona,
Hasa tukiwa wawazi,wagonjwa wote tapona,
Mungu baba mwenye enzi, mjuzi leo na jana,
Ukishaona dalili ,nenda toa taarifa,

Nenda toa taarifa ,uwekwe karantini,
Usije leta maafa,maisha yana thamani,
Kujificha sio sifa , utaleta tafrani,
Kuzifahamu dalili, ndio jambo la muhimu,

Jambo lingine muhimu , mikusanyiko epuka,
Salimia kwa nidhamu,bila mikono kushika,
Msijitoe fahamu,lau sio twawazika,
Korona gonjwa hatari ,halichagui kabila,

Halichagui kabila,hili gonjwa la ajabu,
Virusi havijalala,vipo macho mujarabu,
Japo kuwa una hela ,au japo umetubu,
Chunga usije kupata,kwa wenzio kusambaza,

Chunga usije kupata, korona haina tiba,
Hiki kirusi matata,kinamaliza nasaba
Makabila kinafuta ,yarabi twaomba toba,
Mungu aepushe mbali,dunia iwe salama,

Dunia iwe salama, tuungane binadamu,
Imara tukisimama, korona haitadumu,
Itarudi nyumanyuma, itokomee kuzimu,
Jambo la muhimu kwetu, tufuate taratibu

Korona kigeugeu, hainalo umbo moja ,
wala haitoi ngeu,hicho ni chake kioja
Msije geuka geu, simameni kwa umoja
Kwa umoja wetu sote ,tutaishinda korona,

Wataalamu wa tiba, endelezeni tafiti,
tuiepuke suhuba,kwa dawa tujizatiti,
tiba isiwe ni haba,tuepuke tashititi.
shime kwa jamii yote , kanuni tuzingatie

Tufuate taratibu, korona ipite mbali,
Kutulia ni jawabu, kisha tumwombe jalali,
Litoke lilotusibu,kuziondoa dalili,
Mola muumba jalia ,korona tuepuke.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi
Makao Makuu Dodoma,
5 Barabara ya Uchaguzi,
41107 Njedengwa,
Uchaguzi House,
Anuani: S.L.P 358, Dodoma
Namba ya simu: +255 26 2962345-8
Nukushi: +255 26 2962348
Barua pepe: Uchaguzi@nec.go.tz

www.nec.go.tz tumeyauchaguzi_tanzania

Tume ya Uchaguzi-TZ Tume ya Uchaguzi-tz NEC online TV